JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
SHULE YA SEKONDARI ENDUIMET
WILAYA YA LONGIDO
S.L.P 82 SANYA JUU
SIMU NA: +255 767 383 496 AU +255 782 383 496.

Kumb Na ESS/AD/01/VOL.1/08 **Tar. 11/01/2021**
Ndugu ……
S.L.P ……
……

YAH: MWANAO KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha **I** katika shule ya Sekondari **Enduimet** mwaka huu wa **2021.** Kwa niaba ya walimu na watumishi wengine wa shule ya Sekondari Enduimet, nachukua fursa hii kukupongeza wewe na mwanao kwa kupata nafasi hii muhimu.***HONGERA SANA!***

1.0 MAHALI SHULE ILIPO

1.1. Shule ya Sekondari **Enduimet** iko katika mkoa wa **Arusha** Wilaya ya **Longido** Tarafa ya **Enduimet** Kata ya **Olmolog**, Kijiji cha **Lerang'wa. Ni umbali wa km 60 toka mji wa Sanya juu.**

1.2. JINSI YA KUFIKA SHULENI

Kwa wanafunzi wanaotoka **Longido Mashariki na Namanga** ni muhimu wapitie **ARUSHA** kisha wapande gari la kwenda **MOSHI** na washukie **BOMA NG'OMBE**. Wakifika Boma ng'ombe wapande magari ya kwenda **SANYA JUU** ambapo watashuka na kupanda magari yaendayo **LERANG'WA.** Hapo ndipo mahali shule ilipo. Shule iko kilometa 1.5 toka kituo cha magari ya Lerang'wa.

Aidha nasisitiza sana mwanafunzi afike **SANYA JUU** kabla ya saa **5** (TANO) asubuhi ili kuwahi magari ya Lerang'wa. Shule itaandaa usafiri toka **SANYA JUU** kwenda **LERANG'WA** kwa wanafunzi watakao wahi siku ya kufunguliwa shule, ila mwanafunzi **awe na nauli** ambayo ni **sh. 5,000/= kwa Magari ya aina ya NOAH na HIEACE.**

2.0. UFUATAO NI UTARATIBU WA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ENDUIMET

2.1. Shule itafunguliwa rasmi tarehe **11/01/2021** unapaswa kumleta mwanao siku hiyo bila kukosa.Muda wa kuripoti shuleni ni kuanzia saa **2:00 Asubuhi** hadi saa **11:00 jioni**. Siku ya mwisho kuripoti shuleni ni tarehe **27/01/2021.**

2.2. Mwanao atatakiwa kuja na yafuatayo ili apokelewe shuleni;-

3.0. SARE ZA SHULE

Ndugu Mzazi/Mlezi. Shule ya Sekondari Enduimet itakuwa na sare za aina tatu zitakazotumika na wanafunzi wakati wote wakiwa shuleni. Hii ni kusema kuwa hakuna mwanafunzi atakaye ruhusiwa kuleta shuleni mavazi tofauti na hayo. Sare hizi ni;

3.1. (a) Wavulana.

(i) Sare ya darasani.
- Suruali 2 rangi za rangi Kijivu. Ziwe na Mikunjo Chini (Turn Up). Zenye jina lake kuzunguka Kiuno.
- Socks nyeusi pea 2 na zaidi.
- Mashati 2 meupe. Yenye jina lake kwenye kola ya shati.
- Masweta 2 ya rangi ya Kijivu. Yenye jina lake kuzunguka shingo.
- Tai 2 za rangi ya kijivu kama Sweta na Suruali na zisiwe na mistari. Ziwe na jina lake.

(ii) Sare ya Kushindia.
- Suruali 2 za rangi ya Dark Blue Ziwe na Mikunjo (Turn Up). Zenye jina lake juu ya Mfuko pande zote.
- Fulana 2 za rangi ya Dark Blue Zenye jina lake kuzunguka shingo.
- Masweta 2 ya rangi ya Dark blue Yenye jina lake kuzunguka shingo.

(iii) Track Suit. Zenye rangi ya Kijani kilichoiva na michirizi meupe ubavuni mwa mikono na miguu.

(iv) Mashuka 2 au Zaidi ya rangi ya **KIJANI KILICHOIVA.**

(b) Wasichana.

(i) Sare ya darasani.

- Sketi 2 rangi za Kijivu. Ziwe na Marinda Madogo (Sio Rinda Boksi). Urefu uanzie inchi 5 kutoka Kifundo cha Mguu. Zenye jina lake kuzunguka Kiuno.
- Stockings nyeupe pea 2 na zaidi.
- Mashati /Blauzi 2 nyeupe. Yenye jina lake kwenye kola ya shati/blauzi.
- Masweta 2 ya rangi ya **Kijivu.** Yenye jina lake kuzunguka shingo.
- Tai 2 za rangi ya **Kijivu** kama Sweta na Suruali na zisiwe na mistari. Ziwe na jina lake.

(ii) Sare ya Kushindia.

- Suruali 2 za rangi ya Dark Blue. Ziwe na Lastiki kwa nyuma na jina lake.
- Sketi 2 za rangi ya Dark Blue. Ziwe na Lastiki kwa nyuma na jina lake.
- Fulana 2 za rangi ya Dark Blue Zenye jina lake kuzunguka shingo.
- Masweta 2 ya rangi ya Dark blue Yenye jina lake kuzunguka shingo.

(iii) Track Suit zenye rangi ya **Light Blue** na michirizi meupe ubavuni mwa mikono na miguu.

(iv) Mashuka 2 au Zaidi ya rangi ya **KIJANI KILICHOIVA.**

(v) Wasichana wa Kiislamu waje na Shungi Nyeupe 3 zenye kofia nyeupe (Sio Vitambaa wala Mitandio). Pia waje na Shungi Nyeusi 2 za kushindia.

(c) **Mavazi ya Michezo:** Raba za michezo kwa wachezaji wa mpira wa miguu (Njumu). Raba nyepesi kwa wote (Wasichana na Wavulana) kwa ajili ya Mchaka Mchaka na Mazoezi Mepesi. Bukta na Fulana Nyekundu kwa Wavulana. Bukta na Fulana za Kijani kwa Wasichana (Jezi za Darasa).

4.0. **MAMBO MENGINE MUHIMU KWA WOTE**

4.1. Kwa Wakiristo Waje na Biblia ya Kiingereza na Waislamu waje Msahafu wa Sehemu tatu. (Mungu Kwanza)
4.2. Godoro 3 x 3 ft x 6 futi
4.3. Vyombo vya chakula, sahani, bakuli, kikombe, na kijiko.
4.4. Aje na Begi la kubebea au kuhifadhia vitabu na madaftari.
4.5. Aje na Folda/Jalada la Kuhifadhia Mitihani na Kumbukumbu nyingine.
4.6. Ndoo moja ya maji ya lita 10, kwa matumizi binafsi na kata ya kuogea.
4.7. Dumu la lita 5 la kuhifadhia maji ya kunywa.
4.8. Vifaa vya darasani. Madaftari yasiyopungua 12 (counter books quire 3) rimu 1 ruled na daftari 12 ndogo kwa ajili ya mazoezi ya kushtukiza mara kwa mara, mathematical set, kalamu blu/nyeusi 10, penseli 5 na rula.
4.9. Kamusi ya kiingereza (oxford dictionary).
4.10. Fedha za matumizi (pocket money) kwa ajili ya mwanao na nauli kwa ajili ya wakati wa likizo kwa mwanao.
4.11. Viatu vyeusi vya kufunga na Kamba. Viatu vizuri ni vya Mtumba ili viweze kuhimili Matope Mazito Msimu wa Mvua. Visivyo na visigino virefu wala buti au Plastiki.
4.10. Aje na sanduku la bati gumu (tranka) saizi ya kati lenye kufuli 2 kwa ajili ya kutunzia vifaa vyake kwa usalama.

- ❖ Nasisitiza kuwa ni lazima kila mwanafunzi afike na mzazi au mlezi wake siku ile ya kwanza ya kuripoti kwake shuleni.
- ❖ Ni marufuku kwa mwanafunzi kuja na nguo za nyumbani tofauti na zilizo elekezwa hapo juu.
- ❖ Kila mwanafunzi aje na Jembe, Slesha, na Fagio la Chelewa.

KUMBUKA!

i. Shule haina chakula maalum kwa ajili ya wanafunzi/mwanafunzi wenye matatizo ya tumbo.
ii. Mzazi atapaswa kuchangia shilingi 7000 kwa mwaka kwa ajili ya bima ya afya **(CHF) kwa wasio na bima ya afya ya taifa (NHIF).**
iii. Ikumbukwe kuwa ni lazima fomu hii ijazwe kikamilifu vinginevyo tutashindwa kumpokea mwanao.
iv. Ikumbukwe kuwa shule hii ni ya Bweni kwa Wasichana na Wavulana. Kwa hivyo, mzazi/mlezi kuwa karibu sana na mwanao na watumishi ili kujenga taifa imara.

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, sayansi na teknolojia yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais - TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yamefafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

1. Lazima mwanafunzi kusimama na kumsalimia mwalimu au mtu yeyote aliyemzidi umri anapoingia darasani, ukumbi wa mkutano au anapoingia eneo la shule.
2. Ni marufuku kwa mwanafunzi kutumia lugha chafu wakati wowote na mahali popote.
3. Wanafunzi wakishaingia shuleni hawatatoka, ila kwa **ruhusa ya maandishi** toka kwa **Makamu Mkuu wa shule au mkuu wa nidhamu na malezi.**

4. Wanafunzi waheshimu: wimbo wa Taifa, Bendera ya Taifa, Wimbo wa shule, Picha za viongozi, Fedha za Taifa na Alama nyingine za Kitaifa.
5. Wanafunzi **HAWARUHUSIWI** kwa sababu yoyote ile kutembelea:-
   a. Vilabu vya pombe
   b. Majumba ya starehe
   c. Nyumba za kufikia wageni
   d. Nyumba za walimu.
6. Kila mwanafunzi ni lazima kuvaa sare ya shule (School Uniform) akiwa shuleni na hata aendapo nje ya shule, wakati na muda wa masomo isipokuwa nyumbani wakati wa likizo.
7. Ni lazima na ni wajibu kuwahi kwa kila kipindi cha masomo, kazi au shughuli yoyote ya shule kila wakati.(punctuality)
8. Juhudi katika kazi za mikono, madarasani na katika michezo, ni wajibu wa kila mwanafunzi. Uzembe katika shughuli hizi hauruhusiwi kabisa.
9. Ugomvi au kupigana, Matusi au lugha chafu kwa ujumla na kuleta fujo au kelele madarasani ni mwiko kwa kila mwanafunzi.
10. Kama ilivyo vipindi vya masomo mengine, ni lazima kila mwanafunzi kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparations) na vipindi vyote vya dini ni lazima vitambuliwe na kuhudhuriwa na kila mwanafunzi.
11. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuleta shuleni vitu kama Kamera, Simu za mkononi, Redio, n.k iwapo kuna ulazima kibali kitatolewa na mkuu wa shule.
12. Upole na utii kwa viongozi wote ni wajibu wa kila mwanafunzi, na ubishi wenye lengo la kukwepa kutimiza wajibu ni marufuku.
13. Makoti, Jackets, Vibandiko, Kofia (pamoja na Jungle hats) Kanda mbili, Raba, Yebo Yebo, Mikanda mipana, haviruhusiwi kuvaliwa na mwanafunzi wakati akiwa na vazi la shule (school uniform)
14. Ni lazima kila mwanafunzi kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule. Mwanafunzi haruhusiwi kunyoa kipara/Mitindo ya kihuni (zungu la unga, Kiduku, n.k)
15. Makosa yafuatayo yatasababisha mwanafunzi aondolewe shuleni mara moja
    - Wizi
    - Ulevi wa aina yoyote kama Uvutaji wa sigara na madawa ya kulevya kama vile bangi, cocaine au matumizi ya mirungi, kuberi, n.k.
    - Kupiga au kupigana
    - Kuharibu mali ya umma
    - Kudharau Bendera na wimbo wa Taifa.
    - Kuoa au kuolewa
    - Kupata mimba au kuharibu mimba ndani au nje ya shule.
    - Uasherati na ushoga
    - Ubakaji
    - Migomo ya aina yoyote ikiwemo kukataa adhabu kwa makusudi.
    - Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi.
    - Kukataa adhabu kwa makusudi
16. Kila mwanafunzi ni lazima azingatie ratiba ya shule kikamilifu.
17. Mwanafunzi asiyehudhuria shuleni mfululizo kwa siku 90 atahesabiwa amejifuta shule.
18. Ruhusa ya kutohudhuria shule lazima itolewe na mkuu wa shule.
19. Lugha rasmi ya masomo darasani na nje ya darasa ni KIINGEREZA. Lugha ya KISWAHILI na nyingine za kienyeji haziruhusiwi.
20. Kazi za mikono ni sehemu ya elimu na zinatumika kupima maendeleo ya mwanafunzi shuleni.
21. Ni lazima kila mwanafunzi kutunza mali ya umma.

UFAFANUZI WA SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Mwanafunzi akisharipoti shuleni, haruhusiwi kutembelea maduka au majumba ya starehe. Haruhusiwi kuzurura ovyo maeneo ya shule au nje ya shule wakati wa masomo. **Ruhusa** ya kutoka na kulala nje ya shule inatolewa na **Mkuu wa shule**. Ruhusa za **kwenda na kurudi** hutolewa na **Makamu Mkuuwa shule** (**Gate Pass ya maandishi**). Masomo, michezo, na kazi ndizo nguzo za malezi shuleni. **LAZIMA KUSHIRIKI KIKAMILIFU**.

Shule ina taratibu za kidemokrasia za kufikia maamuzi, serikali ya wanafunzi, kamati mbalimbali, baraza la shule, - School Council- Maoni na mapendekezo yatolewe humo. Aidha vikao vya madarasa hutumika kutoa maoni ambayo yatafikishwa

ngazi zinazohusika kwa uamuzi na utekelezaji. **SANDUKU LA MAONI** pia laweza kutumika kutoa dukuduku **MAONI HUZINGATIWA.**

Mwalimu wa darasa ndiye mlezi wa karibu katika maendeleo ya nidhamu na taaluma. Wanafunzi wawe wazi kuwatumia waalimu wa madarasa kueleza matatizo yao na kero zao bila woga wala kusingizia. Wawe wakweli. Serikali ya wanafunzi huchaguliwa na wanafunzi wenyewe. Wanafunzi wanahamasishwa kushiriki katika kugombea nafasi za uongozi na pia kuchagua kwa uhuru. Kura huwa siri.

Kila mwanafunzi sharti atunze vifaa vyote anavyopewa. Utunzaji wa mali ya umma na ile ya binafsi, huwa kigezo katika kupima tabia. Kila Jumatatu asubuhi majaribio hufanywa darasani. Haya huwa sehemu ya tathimini ya mwisho wa muhula. Wazazi wanayo haki ya kuona karatasi za matokeo kuchunguza daftari za wanafunzi na kuwasiliana na walimu wa madarasa wanapoona dosari. Mwanafunzi atakayekosa kufanya majaribio ya kila Jumatatu bila sababu atarudishwa nyumbani.

Kila mzazi amtosheleze mtoto wake mahitaji yote ya Afya, Vitabu, Madaftari, Kalamu. **RIPOTI** ya mwisho wa muhula ni haki ya mzazi. Mzazi ahakikishe anaipata na kuichambua ili kumhimiza, mtoto wake anapoonyesha maendeleo duni ya masomo na tabia.

"WATUMISHI NA WANAFUNZI WANAZO DINI KIMADHEHEBU. KWA HIVYO, MWANAFUNZI AKIRIPOTI AJITAMBULISHE KIDINI NA KIDHEHEBU KWANI KUHUDHURIA VIPINDI VYA DINI KWA RATIBA NI LAZIMA KWA WANAFUNZI WOTE. NA KAMA HANA DINI AU DHEHEBU ATAPEWA UTARATIBU."

KAULI MBIU YETU! ELIMU NI MSINGI WA MAENDELEO!

Asante sana na nakutakia mafanikio mema katika safari hii ya kuandaa vema maisha yako.

Karibu sana shuleni Enduimet sekondari

HASSAN HAMISI HASSAN

MKUU WA SHULE – ENDUIMET SEKONDARI

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
SHULE YA SEKONDARI ENDUIMET
WILAYA YA LONGIDO
S.L.P 82 SANYA JUU
SIMU NA: +255 767 383 496 AU +255 782 383 496.

FOMU YA "UTII NA TABIA NJEMA"
TAMKO LA MWANAFUNZI

Mimi _____, nimesoma sheria za shule na taratibu zote. Naahidi kuzitekeleza kwa ukamilifu mkubwa na kufuata ushauri wa waalimu.
Nitahudhuria masomo yote kila siku, na kufanya mazoezi, majaribio yote na mitihani yote kikamilifu. Sitashiriki katika hila zozote za wizi au udanganyifu wa mitihani. Nitashiriki katika klabu za kimasomo na michezo mbalimbali shuleni.
Michezo ninayoshiriki vizuri ni 1._____
2. _____ 3. _____
Naweza kushiriki vyema katika fani za ndani katika 1. Kwaya ( ) 2.Ngoma ( ) 3. Maigizo ( ) 4. Ngonjera ( ) 5. Muziki ()
[weka alama ya (√)***kubainisha unavyoweza kushiriki]***
Nitashiriki kikamilifu katika kazi zote za mikono. Natambua kuwa migomo na vurugu ni haramu hivyo sitashiriki wala kushawishi wengine kujihusisha.
Nitawasirisha matokeo ya mitahani na majaribio pamoja na barua nitakazopewa shuleni kumpelekea mzazi/mlezi wangu.
JINA LA MWANAFUNZI_____
SAHIHI_____
TAREHE _____

SEHEMU A: HABARI ZA MWANAFUNZI

1. Jina kamili (**kama kwenye mtihani wa kumaliza elimu ya msingi**)
   _____
2. Tarehe ya kuzaliwa _____ Dini _____Madhehebu _____
3. Mahali na wilaya alipozaliwa _____
4. Shule ulipo hitimu darasa la saba / kidato cha _____
5. Kidato unachokuja kujiunga shuleni _____
6. Majina ya vyama vya masomo mbalimbali ambavyo umewahi kujiunga
   1. _____
   2. _____
   3. _____
   4. _____
7. Michezo au ngoma unazopendelea
   1. _____
   2. _____
   3. _____
   4. _____
8. Kazi yoyote ya uongozi uliyowahi kufanya kama vile kiongozi wa michezo, kwaya, ngoma, kiranja, maktaba n.k

MADARAKA/ UONGOZI	SHULE/MAHALI	MWAKA

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
SHULE YA SEKONDARI ENDUIMET
WILAYA YA LONGIDO
S.L.P 82 SANYA JUU
SIMU NA: +255 767 383 496 AU +255 782 383 496.

FOMU YA KUJIANDIKISHA SHULENI NA HABARI ZA MZAZI/MLEZI

SEHEMU B: HABARI ZA MZAZI / MLEZI

1. Jina kamili la Baba _____
2. Kazi yake _____
3. Jina kamili la mama _____
4. Kazi yake _____
5. Jina kamili la mzazi/ mlezi (iwapo mtoto haishi na wazazi wake)_____
6. Kazi na Anuani ya mlezi _____
7. Namba ya simu _____
8. Nyumbani kwa Baba (Alipozaliwa mtoto) _____ Kijiji/ Mtaa _____ Wilaya _____ Kata _____
9. Mahali pa kazi pa Baba _____ Simu _____
10. Mahali pa kazi pa Mama _____
11. Mtoto anaishi na (i) Baba (ii) Mama (iii) Wazazi wote (iv) Mlezi [kata isiyostahiki]
12. Dini ya Baba _____ Madhehebu _____
13. Dini ya Mama _____ Madhehebu _____
14. Madhehebu utakayo mwanao alelewe _____
15. Anuani kamili ya nyumbani ambako mtoto atakuwa anakwenda siku za likizo _____
16. Mimi _____ Baba/Mama /Mlezi wa _____ nathibitisha kuwa taarifa hiyo hapo juu ni sahihi na naahidi kushirikiana na walimu ili kuhakikisha kwamba mwanangu anakuwa na tabia nzuri, na mwenye bidii ya masomo.

Sahihi ya Baba/Mlezi _____

Tarehe _____

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
SHULE YA SEKONDARI ENDUIMET
WILAYA YA LONGIDO
S.L.P 82 SANYA JUU
SIMU NA: +255 767 383 496 AU +255 782 383 496.

MINISTRY OF EDUCATION, VOCATIONAL TRAINING, SCIENCE AND TECHNOLOGY

FOMU YA TAARIFA ZA KIAFYA ZA MWANAFUNZI

Fomu hii ijazwe na afisa wa afya wa kituo cha afya cha serikali na irejeshwe shuleni siku ya kumleta mwanafunzi

Full Name _____
Age _____

1. AIDS Test _____
2. Blood count (red & White) _____
3. Urine examination _____
4. Stool examination _____
5. Syphilis Test _____
6. TB Test _____
7. Ear Test _____
8. Eye Test _____
9. Abdomen _____
10. Spleen _____
11. Additional Information or any other Physical, Mental hereditary or infectious diseases:-

_____

_____

(Please state nature of treatment)

Medical certificate:

I certify that the above mentioned has been examined and found it to / not to pursue further education

Signature _____

Designation_____

Station_____

Date_____ Official Stamp _____